



# Sala za siku kenda ya matayarisho kwa siku ya kuwatangaza wenye-heri mashahidi

Uvira (RD Congo) 18.08. 2024

# Mpango wa sala

UTANGULIZI

Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amen

SOMO FUPI

*Inabadilika kadiri ya siku*

SOMO LA KIKSAVERIANO

*Inabadilika kadiri ya siku*

KUFIKIRI

*Inabadilika kadiri ya siku*

MWISHO

Tusali kwa maombezi ya Mashahidi wa Baraka na Fizi:

Baba Mtakatifu, mwenyi huruma tele,
wewe umeipatia Eklewya yako Waksaveriano
Vittorio Faccin, Luigi Carrara,
Giovanni Didonè na abbé Albert Joubert,
wachungaji na mitume kadiri ya Moyo
wa Mwana wako Yesu Kristu.

Wakiwaka moto wa mapendo,
hawakuacha kundi la kondoo katika hatari
bali walibaki kulilinda mpaka kumwaga damu,
wakiungama jina la 'undugu usio na mipaka'.

Kwa maombezi yao, utujalie neema
tunayokuomba kwa unyenyekevu...
Kwako sifa na utukufu milele na milele. Amen.

Bwana atubarikie, atukinge na maovu yote na kutufikisha kzenyi Uzima wa Milele. *Amen*

Wote wamjue na kumpenda, *Bwana wetu Yesu Kristu.*

Mtakatifu Guido Maria Conforti na Mtakatifu Fransisko Xaveri, *mutuombee.*

# Siku ya kwanza (09.08.’24)

*Kujitolea*

## SOMO FUPI

WaRoma 12, 1-2

Ndugu zangu, nawasii, kwa ajili ya huruma yake Mungu: mutolee miili yenu kuwa sadaka takatifu, yenye uzima, yenye kumpendeza Mungu: ndiyo ibada yenu ya kiroho. Msishike mwendo wa dunia hii, bali mgeuke kuwa watu wapya, wenye mawazo wapya, mpate kutambua mapenzi ya Mungu, mambo gani ni mema na yenye kumpendeza na makamilifu.

## SOMO LA KIXAVERIANO

Lapatikana katika «Hotuba kwa washika-safari ya Missioni» za Mt Guido Maria Conforti, askofu

(*Neno la mwanzishi*, Parma 1966, 102-106; Disc. 12, katedrale ya Parma, 16.11.1924)

*Mujitolee bila kipimo kwa ajili ya mema ya watu*

“Missionaryo binafsi ni mfano mkuu na bora zaidi ya maisha makamilifu. Yeye atazama kiroho sura ya Yesu Kristu anayewaonyesha Mitume dunia tunayopashwa kushinda na kuifikisha kwa Enjili, siyo kwa nguvu ya silaha, ila kwa kukubalishwa na mapendo, nayo yashika watu. Naye kwa ajili ya makusudio hayo, anajitolea mpaka kuacha jamaa yake, nchi yake, yale yenye kumpendeza zaidi na yaliyo halali, kwa nia moja tu ya kutafuta na kupata watu wanaofikishwa kumwamini Kristu; habebi upanga wala bunduki kwa kushinda magumu ao vizuio vya njiani, ila akibeba silaha tu ya Msalaba ya Yesu Kristu, tayari pia kwa kumwaga damu ikiwa ya lazima kwa ajili ya mema ya wandugu, zaidi, ndani ya moyo wake anatamani ushahidi wa kifo hicho kwa kufunga utume wake. (…)

Utume wenu uendelee, ulete sifa na hasa utoe matunda mengi ambayo yatakuwa mshahara wenu juu ya mambo yote muliyoacha. Kikombe munachoanza kunywa ni kikombe cha Jetsemani:

hamutakosa mateso na magumu; Shetani, Mkuu wa giza, ambaye ufalme wake munatafuta kuangusha, hataacha kitu katika mashambulizi ya kuzuia njia yenu; kwa ubaya wa binadamu, itafurika juu yenu zoruba ya mazulumu na chuki sababu ya Jina la Yesu: mutaonja yale aliyoyaonja Paulo, Mtume wa mataifa, aliyewatangulia katika njia tukufu ya kuenjilisha mataifa. Lakini, katika Neema ile iliyomwimarisha Paulo, nayo itawaimarisha nyinyi pia katika mapigano hayo makali. Nyinyi munavaa Yesu Msulubiwa aliye upanga wenu, nguvu yenu, silaha isiyoshindika, siri ya ushindi wenu. Msalaba huo utawafanya wakubwa zaidi kuliko uzaifu wenu, mutashinda mabaya yote ya kipagani na kusonga mbele kwa kueneza duniani Ufalme wa Mungu katika amani".

## Mafikiri

*Yametolewa na P. Fernando García Rodríguez, mkuu wa Waxaveriano wote*

Maisha ya kitume yakuta, katika ushahidi wa kumwaga damu maonyesho wazi zaidi ya kuiaminia Enjili. Kutoa naziri kwa kujitolea lote kwa Bwana ni alama ya kuweka yote katika mikono yake.

"Akimfuata Kristu, katika Jamaa Xaveriana, kila Mxaveriano anaitwa kujitoa wote yeye mwenyewe kwa Enjili ya Ufalme katika utakatifu wa maisha mpaka saa ile ya kumwaga damu" *(Sheria ya Utume Xaveriano 17)*.

Wenzetu Faccin, Carrara, Didonè na Joubert walikuwa wanadamu sawa kawaida, wenye fazila na vilema, lakini hasa wenye kuwaka kabisa moto wa kueneza Ufalme wa Mungu. Japo uzaifu wao wa kibinadamu, walimpenda Mungu kwa moyo wote na kwa roho yote na kwa akili yote na utashi wote; na hivi walikuwa-wapenda raia na nchi ya kikongomani, ambamo Mungu mwenyewe aliwatuma. Mapendo hayo kwa Mungu na kwa WaKongomani yalikuwa makubwa na yenye kukamata pande zote za uzima, mpaka kufika na uhodari kwa kitambo cha kutisha kweli chenye kuwangojea. Ndio ushahidi bora wa maisha ya kikristu! Ndio urisi mzuri kwetu sisi wote!

# Siku ya pili (10.08.'24)

*Kufaidia Kristu*

## Somo fupi

WaFilipi 3, 7–8

Ndugu zangu, yaliyokuwa faida kwangu, naliyaona kuwa upotevu kwa ajili ya Kristu. Na kweli naona mambo yote ni upotevu, nikiyafananisha na faida kuu ya kumjua Kristu Yesu Bwana wangu. Kwa ajili yake yeye, nimependa kupotelewa na yote nikiyaangalia kama takataka, ili nimpate Kristu.

## Somo la kixaveriano

Kutoka "Barua kwa Wazazi" ya P. Luigi Carrara, padri na shaidi

*(Kitabu cha barua, Roma 2024, 72; Parma, 01.01.1962)*

*Missionaryo anaondoka akilinda mapendo ya jamaa yake ya kuzaliwa*

"Mufurahi, muchangamuke, mushangilie na miye kwani habari njema moja na zawadi kubwa imenifikia na sherti niwaelezee nyinyi!! Wakubwa wetu wananituma katika Missioni! Kongo inaningoja! Mwaka 1961 umeniome Padri, na 1962 utaniona katika Nchi ya Utume! Nimeitwa kulima shamba la mizabibu la Bwana, kutumika shamba nzuri zaidi, lenyi kubeba matumaini ya kupendeza zaidi na pia lenyi kuwa na shida zaidi.

Kongo inaonyesha alama za ujio wa wakati bora wa kikristu, ikiwa nguvu zetu nyingi zitafika huko bila kuchelewa... isipokuwa hivi, itakuwa nyuma mno. Kumbe mimi naitwa kuenda kule, wakati huu wa lazima sana, saa hii kuu kabisa, ndiyo maana navimba moyo kwa furaha na kumshukuru Bwana kwa roho yangu yote. Ngambo yenu nyinyi mujiunge nami kwa kumpigia aksanti. Hiyo ndiyo habari njema iletayo na mwaka mpya na inatokea kwa mapendo ya Bwana Yesu Kristu".

## Mafikiri

Ya Lisa Zuccarini, aliyeandika maisha ya Mashahidi wetu

Nakumbuka moyo mzuri wa Luigi Carrara, alipokuwa akitayarisha safari ya kuenda mu Kongo mwaka wa 1962. Alikuwa akisikia huzuni ya wajamaa yake, alikuwa anaona mawazo ya mama aliyemwaza kama anakufa ginsi fulani, pale katika nchi ya watu wengine waliokuwa tayari kumpokea. Mungu anaomba hatua muhimu kwake na pia kwa mioyo ya wazazi wake wanyonge. Mungu anajua ginsi wajamaa wake walijikatalia kwa kumkomalisha, na Yeye anawashukuru zaidi leo. Anawaakikisha wote kuhusu heri na furaha yake, anawaalika kusali na kufurahi pamoja. Luigi yupo na uhakika kamili, na hivi anataka wazazi wajipe moyo: Mungu anastahili kuaminiwa, anajaza tuzo bila kipimo, hakuna kitu tunachotolea kwa Jina lake kinachoweza kupotea, zaidi sana akitolewa mwana mzima.

Wakati wa kukumbatiana na mama, kabla ya kuondoka, kuelekea Kongo, ilikuwai ya huzuni kubwa kabisa. Elisabeti alizidi kulia machozi, akijisikia moyoni kwamba hii ni mara ya mwisho ya kumkubatia Luigi mpenzi... Alizidi kusema ‘Sitakuona tena! Sitakuona tena!’.

# Siku ya tatu (11.08.'24)

*Utiifu na mapendevu*

## Somo fupi

Fil 4, 8.9b

Ndugu zangu, fikirini mambo yote yaliyo kweli, yote yaliyo heshima, yote yaliyo haki, yote yaliyo safi, yote yaliyo mapendevu, yote yaliyo na sifa njema, yote yaliyo na fazila na ya kusifiwa. Mambo yaliyofundishwa nami na kuyapokea kwangu, na kuyasikia na kuyaona katika mwendo wangu, fanyeni hayo. Naye Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi !

## Somo la kixaveriano

Limetoshwa katika Hadisi ya maisha ya Albert Joubert, Padri na Shahidi

(Emilia Flocchini, Albert Joubert, http://santiebeati.it)

*Utiifu na Mapendevu: fazila mbili za Albert Joubert*

"Katika mwendo wa ya kuiendea Upadirisho, Albert alitumika sana juu ya tabia yake, kwa kuigeuza kuwa nyenyekuvu na ya kufaa. Alijulikana kama mwana wa Kapiteni Joubert, lakini heshima ya watu ilikuwa mbali na moyo wake; yeye alitamani kukomaa katika utii na katika hamu ya kuleta mafaa kwa wengine.

Baada ya kupadirishwa, tarehe 6.10.1935, Padri Joubert alijiweka tayari kuenda katika missioni za mbali zaidi. Kwanza alitumwa Kasongo, 750 Kilometri mbali na Baudoinville. Halafu alitumika katika missioni mbalimbali nane. Kwa kufika katika miji ya mbali zaidi, alitembea na miguu siku nyingi na hivi apate kuwaletea Masakramenta, kuwafundisha zaidi wakatekista katika elimu ya enjili na kuwapa moyo wa kujitolea. Alipotumwa katika seminari ndogo ya

Lusaka na ya Mungombe kuwa mwalimu, alikuwa tayari kusaidia wenzake Mapadri, katika kazi ya kitume, hasa pa nyakati za nguvu zaidi kama vile majilio na kwarezyma. Na popote fazila ya pekee yake ilikuwa roho ya urafiki na ya mapendevu kwa ajili ya wote: kwa kila mmoja alikuwa anaona heshima".

## Mafikiri

Ya P. Gabrieli Basuzwa Lusunwa, Xaveriano

Kama vile wenzake mashahidi wa Fizi na Baraka, kwa kweli, Albert alimkabisi Mungu maisha yake, akijitolea pamoja na wale ambao tangia miaka mingi waliishi katika magumu ya Kongo.

Albert alikuwa wazi na mwenye haki. Kwa sababu hiyo aliona furaha ya kuishi ginsi angavu na kustahili kuheshimiwa na jirani. Alifanya bidii sana kwa kujipatia unyenyekevu, na hiyo pia sababu ya akili yake wazi na ya upokelevu wa wale aliowekwa na Mungu katika njia ileile yake.

Aliadibishwa katika masomo bora zaidi kuliko yote ya wakati ule, seminari ndogo ya Lusaka na seminari kubwa ya Baudoinville. Albert alitoa maadibisho bora kwa vijana na watu wengine wa Taifa la Mungu, walioaminiwa kwake. Utambuzi wake ulikuwa juhudi ya kitume na mpendevu yake.

Katika mwili wake na katika maisha wake, Albert alibeba mwungano wa utamaduni mbalimbali (interculturalité) na ushirika kati ya mataifa. Baba yake alikuwa Mfransa na mama Mkongomani na wote wawili waliishi fazila za kienjili yenye kuunganisha makabila mbalimbali. Furaha ya kuishi kwa daraja sawa, heshima ya kuwa waana wa Mungu, katika Joubert ni alama ya cheche ya umilele wa mtu aliyeumbwa kwa mfano wa Utatu Mtakatifu.

# Siku ya nne (12.08.’24)

*Kupenda kwa moyo wote*

## SOMO FUPI

Mt 28,16.18-20

Wale wafuasi kumi na mmoja walienda Galilea mpaka mlima ule walioagizwa na Yesu... Yesu akawajongea akawaambia: «Nimepewa uwezo wote mbinguni na duniani: basi, nendeni mkafanye mataifa yote kuwa wafuasi, mukiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, na kuwafundisha washike yote niliyowaamuru nyinyi. Na tazameni, Mimi nipo pamoja nanyi siku zote, mpaka mwisho wa dunia.

## SOMO LA KIXAVERIANO

Katika “Barua kwa wazazi” ya Luigi Carrara, Padri na Shahidi

(*Epistolario*, Roma 2024, 171-172; Fizi, 11.02.1964)

*Kupenda Enjili: mchoko na furaha katika*

Padri Luigi anahadisia safari yake ya kwanza, safari katika miji ya milima ya Fizi; ilidumu siku kumi.

“Padri Giovanni, kabla ya kuondoka ameniambia: ‘Utafika bila nguvu, kama mfu: usiungamishe kwanza’. Lakini namna gani kuwaambia watu ‘Hapana sasa’? Walikuwa wakatekista na wengine wa karibu, walionisihi: ‘Padiri, kesho watu watakuwa wengi sana, watatoka ngambo zote, utakosekana wakati: utuungamishe sasa’. Niliitika. Bila kubadilisha hata nguo zenye kujaa jasho, nilikamata kiti, kila mwamini akipiga magoti juu ya udongo, tumeanza. Walikuwa wachache na pa saa moja na nusu ya usiku (19h30) wameniacha. Mimi nimetokotesha, katika chungu kidogo, maziwa waliyonipa. Halafu ningalitamani kusali na baadaye kulala usingizi. Lakini pa saa mbili ya

usiku (20h00) wamegonga mlangoni. Ni wajirani wanaoshika nafasi ya kuongea na Padri, na kuuliza habari nyingi... Wameniacha pa saa tatu na nusu ya usiku (21h30). Ndipo natimiza mambo yangu na kulala".

## Mafikiri

Ya P. Bernard Cibambo, Xaveriano

Inapokaribia sikukuu ya kuwatangaza Mashahidi wetu 'WENYE HERI', ni vizuri kukaa mbele ya picha lenye kuwaonyesha wote pamoja. Hapo twaweza kutambua roho iliyowaongoza watimize ile Missioni ya furaha na ya magumu waliyopewa na Yesu. Katika tafauti za tabia zao, walishirikiana katika moto wa kuambatana na karama ya Mt Guido Maria Conforti: 'Kuifanya dunia jamaa moja / Faire du monde une seule Famille'. Haikuwa neno la kijuujuu! Wakiaminia utume wa Kristu aliyesema "NENDENI", na wakiongozwa na Roho Mtakatifu, Kongo iligeuka kuwa nyumba yao.

Tunaposoma hadisi za safari zao, sawa hiyo ya P. Luigi, tunatambua roho yenye kuwaongoza. Makumi ya kilometri kwa siku, walizoea kutembea kati ya milima. Kwa kuishi kikristu-kitume, sherti pia kupanda milima kwa kuwaendea wandugu na wadada wanaongoja wakiwa na kiu yao ya Mungu.  Japo uchoko wa safari ndefu, Luigi palepale alikuwa tayari kusikiliza... Tendo jema linalofanyiwa kwa ajili ya Enjili lina bey ya umilele. Ushaidi wa kumwaga damu ya Padri  Luigi na wenzake ni utimilifu wa matendo mengi ya kujikatalia na wa kuchagua siku kwa siku yaliyo mema zaidi. Ushahidi wao utusukume kuishi kweli kikristu kila siku.

# Siku ya tano (13.08.'24)

*Kudumu*

## Somo fupi

WaRoma 8,28.35.37-39

Twajua ya kama mambo yote yaleta mema kwa wale wanaompenda Mungu, ndio wale walioitwa kadiri ya kusudu lake... Nani atatutenga na mapendo ya Kristu? Ati ni taabu , ao misongo ya roho, ao mazulumu, ao njaa, ao uchi, ao hatari, ao upanga?...Lakini mambo hayo yote tunayashinda kabisa kwa nguvu yake yeye aliyetupenda. Nina hakika kama wala mauti, zala uzima, wala Pepo, wala Watawala, wala mambo ya sasa, wala mambo yatakayukuja, wala Wenye uwezo, wala Nguvu za juu, wala za chini, wala kiumbe chochote kingine, hakitaweza kututenga na mapendo ya Mungu, katika Kristu Yesu, Bwana wetu.

## Somo la kixaveriano

Katika "Barua kwa binamu Viktorina" ya Vittorio Faccin, mtawa na shahidi

(*Epistolario*, Roma 2024, 171; Baraka, 26.12.1963)

*Kudumu tukitenda mema ni alama ya mapendo maaminifu*

"Dada mpenzi,

Bwana anataka tena kupima mapendo yako kwa ajili yake. Katika majaribu hayo, uwe hodari, vumilia yote katika mapendo yake ili neema nyingi zishuke juu ya jamaa yako, hasa juu ya watoto. Hakuna waridi bila miiba. Katika waridi, tafuta tu uzuri na harufu tamu: uzuri na harufu zakusahaulisha mapigo ya miiba. Maisha yetu kwa ajili ya Yesu yapashwa kuwa mapendo tu. Bwana anataka roho yako iwe nzuri zaidi, safi zaidi, mtakatifu zaidi, labda kwa hiyo amekuitikia mateso na mapendo. Hivi amekupa wakati wa kusali na kufanana naye kila siku zaidi.

Mimi nitakukumbuka wewe katika sala zangu, pamoja na mume wako na waana wako, ili nao wawe na nguvu ya kuvumilia yote kwa mapendo ya Yule Mungu aliyejifanya mtu kwa kutujua na kutupenda zaidi.

Naungana nayi katika Yesu na Maria Mama wa mbinguni".

## Mafikiri

Ya P. Alfonsus Widhiwiryawan, Xaveriano

Kati ya majaribu na magumu, katika hatari na mambo yasiotambulika, sisi wamisionari tunasikia upweke, kuachiliwa, ukosefu wa msaada wa kiroho, mawazo ya kushindwa. Barua kwa WaRoma inatuomba 'tuwe washidaji' katika magumu. Namna gani?

Kwanza, Bwana hakubali tujaribiwe kushinda nguvu zetu, kwani Yeye awajalia wote neema zake (Rm 8,37). Kwa nguvu zangu tu, hakika ningeanguka. Nikijiaminia kwake 'yote yaleta mema' (Rm 8,28). 'Naweza yote katika Yule anayenipa nguvu' (Fil 4,3).

Halafu, tunashinda "tukigeuza yote kuwa takatifu". Mt G.M. Conforti alisema: "Adui mbaya zaidi wa matendo yetu ni kiburi. Tunapashwa kuyafanya matakatifu pia matendo madogo kama pumziko, usingizi, kula, michezo" (Kwa vijana wa novisyato, 04.05.1921). Mbele ya mashindano ya siku hizi, mara nyingi twajifunga ndani mwetu na polepole twajenga kibambazi cha kututenga na wengine. Vittorio anatuomba tusiogope miiba: inatutakasa na kuzifanya roho zetu 'nzuri, safi na takatifu zaidi'.

Mwisho, tunashida 'tukibadilisha maelekeo' ya tanga ya merikebu yetu, kwa kuenda ngambo ya Roho Mtakatifu. Mara kwa mara twajifanya wapinzani sisi wenyewe, tukitegemea nguvu zetu. Conforti atukumbusha kwamba 'kudumu' ni neema tunayoomba: "Ombeni neema ya 'kudumu': ndiyo neema kubwa iliyo taji la vyote" (Kwa wanovisyo, 15.06.1921).

# Siku ya sita (14.08.’24)

*Kindugu*

## SOMO FUPI

WaKol 3, 10-11

Mumevua mtu wa kale na matendo yake, mukamvaa mtu mpya anayeongeza upya wake, kwa mfano wa Mwumba wake. Hapo hakuna tena Mgreki na Myaudi, hakuna aliyetahiriwa na asiyetahiriwa, hakuna mshenzi na Mskite, hakuna mtumwa na mtu huru, bali Kristu ni yote na katika wote.

## SOMO LA KIXAVERIANO

Katika “Barua kwa wazazi” ya Vittorio Faccin, mtawa na shahidi

(*Epistolario*, Roma 2024, 136-137; Mutesa, 15.05.1962)

*Undugu bila mipaka*

“Tarehe 12.04.1962 nimeitwa Mutesa, kwenyi Seminari kuu ya Bukavu, ili nikomboe kwa muda fulani, mweni kazi ya kuweka-feza.

Waseminasti ni 46, wote Wakongomani. Walimu ni Mapadri Weupe Wabeleji watatu, Frera mmoja yeye pia Mbeleji, Padri mwengine Mfransa, halafu kuna Abbé mmoja Mkongomani, na, kwa kufunga daftari, mimi Mwitaliano. Ginsi munaona, hapa tuko wa nchi mbalimbali nne. Lakini kati yetu hakuna Mfransa ao Mbeleji: tunapendana wote! Wakati wa michezo ao mazungumuzo tuko pamoja na hata mara moja husema: ‘Mimi niko...’.

Mapendo ya Yesu yatusahaulisha kwamba tuko Wafransa ao Waitaliani. Wote tunasema kifransa. Halafu mimi, mara nyingi napata nusu ya wakati kwa kujifunza Mashi, iliyo luga ya hapa. Kuna pia wenyi kujua Kiswahili, lakini sio wote”.

## Mafikiri

Ya P. Cesar Da Silva, Xaveriano

Yapata miaka makumi manne, kabla ya kuondoka kwa waana wake wa kiroho, kuelekea nchi itakayosafishiwa na damu yao, Mt Guido Maria Conforti, alikaza neno moja lililo la daima katika maisha ya missioni: undugu. Mt. Guido alisema: "Undugu wasitawi kivulini mwa Msalaba wa Yesu Kristu" (Kwa 'Unione Missionaria del Clero', 20.08.1922).

Msalaba ulikaa daima mbele ya macho ya ndugu zetu Mashahidi. Mbele ya Msalaba walijifunza kushinda mipaka yao binafsi na kuyaendea kwa uhodari mashindano ya wakati wao. Undugu huu utokao msalabani umewafanya mifano ya undugu yenye kuvuta watu: "Nitakapoinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote kwangu" (Gv 12,32).

Juu ya msalaba "mapendo ya Yesu yasahulisha" (Faccin) tafauti zinazotuzuia kuishi kama ndugu kati ya watu wengine. Faccin, Didonè, Carrara na Joubert, kwa damu yao iliyomwagika, ni mashahidi wa "undugu uchipukao kivulini mwa msalaba wa Kristu".

# Siku ya saba (15.08.’24)

*Kujitolea kwa Maria*

## Somo fupi

Yesaya 61, 10

Ninafurahi sana katika Bwana, roho yangu inamshangilia Mungu wangu. Maana amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika bushuti ya utakatifu... kama bibi arusi anavyojivika yohari na mapambo yake.

## Somo la kixaveriano

Katika “Barua kwa ndugu Severino” ya Giovanni Didonè, Padri na shahidi

(*Epistolario*, Roma 2024, 107; Locasca, 10.07.1958)

*Kuaminia Maria: “Pamoja naye tu twaweza kuendelea”*

“Ujipe moyo, kwani wakati wapita mbio sana na hatuwezi kuitika upite bure.

Nakusii, upeleleze uchaji kwa Bikira Maria, kadiri ya Kitabu ‘Uchaji halisi kwa Bikira Maria’, kilichoandikwa na Mt. Grignon de Montfort; ndiyo ginsi kamili kwa kuwa wote wa Maria na, kwa nja yake, kuwa wote wa Yesu.

Pasipo uchaji imara na tamu kwa Maria, hatuwezi kuufikia ukomo wetu wa sifa; zaidi ya vile, nasema: pamoja na Maria tu tunaweza kuendelea.

Nakukumbuka katika sala”.

## MAFIKIRI

Za María Guadalupe Pacheco Rodríguez, Xaveriana

Maria, sawa na mama, sikuzote ni tayari kutusindikiza na kutuongoza katika njia ya imani, ya matumaini, ya amani na pia ya taabu. Tukitembea na Maria, msalaba tunaobeba hautafutika, lakini Yeye akiwa pamoja nasi na kwa maombezi yake, tunapata mwangaza na kuona samani yenye kutufungulia Ufalme wa Mbingu.

Tumwangalie tukiwaza ginsi yeye angetenda pahali petu katika mambo mbalimbali tunayoendea, na polepole tutafikia kufanana naye, vile kama waana wafanana na mama yao.

Sisi pia tumepata Roho Mtakatifu, upaji wa Mungu, ndiyo maana hatuzezi kuitika ife kwetu matumaini ya kufikia utakatifu tukibaki waaminifu kwa ubatizo wetu mpaka mwisho. Kuona Maria karibu na Yesu kwatuambia kwamba tuko wasafiri njiani; havitakosekana taabu, mateso, uchungu, kutotambulikana... Japo ile yote, furaha ya ndanindani ya moyo wa kumtumikia Bwana na kuwa naye saa zote, itatusindikiza daima na popote !

# Siku ya nane (16.08.'24)

*Kushurulikia*

SOMO FUPI

2 WaKor 1, 3-4

Atukuzwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristu, Baba mwenye huruma nyingi na Mungu wa kitulizo che kila aina. Maana anatutuliza katika taabu zote, kusudi tuweze nasi kuwatuliza wenye taabu mbalimbali, kwa kitulizo kile tunachopewa na Mungu sisi wenyewe.

SOMO LA KIXAVERYANO

Barua kwa katekista Rafaeli, ya Padri Giovanni Didonè, Padri na Shaidi

(*Epistolario*, Roma 2024, 422; Lett. del 09.11.1964)

*Utumishi wa kitulizo: kushurulikia moyo*

"Aksanti kwa barua yako na kwa kazi unayotimiza. Sasa kule Roma, katika mtaguso wa Vatikano, walitoa ruhusa kwa Maaskofu wa misioni, ya kuweka mashemasi wawe wasaidizi wa Mapadri; maana yake Askofu anaweza kuchagua wakatekista wenye maisha ya haki na uaminifu na juhudi, wapate ruhusa ya kubatiza na kukomunisha waamini (…) Hayo nakuandikia kwa kukupa kitumaini katika nyakati zijazo. Muvumilie kidogo tu na mtakuwa na Shemasi kwenu. (…). Sisi Mapadri tuko hapa Fizi, mbali sana na nchi zetu, lakini Mungu ni popote na anatuangalia. Twabaki imara! Musiwaze kama Mapadri watarudia nchini mwao, mujue kwamba hao wanapenda kufa kuliko kuwaacha nyinyi. Musifuate wongo za watu. Sisi tumetumwa katika missioni ya Fizi kwa kukaamo. Mimi sijafika bado kwenu kwa sababu siwezi, ginsi nyinyi munajua vizuri sana, nanyi mutaniona, sijui wakati gani, lakini mutaniona ".

## Mafikiri

Ya P. Robert Kowa Sado, Xaveriano

Barua hii ya P. Giovanni Didonè inatujulisha daraja ya upendo wa kitume kwa ajili ya missioni na kwa ajili ya ile sehemu ya taifa la Mungu ambamo yeye alitumwa. Kijana huyu shaidi alijikamata kama chombo cha kitulizo na cha ushirika, kwa namna ya kuishi ya watu, na hivi aliwapa uhakika wa umoja wa maisha na wa ukomo. Usikivu huo wagusa moyo na kuonyesha nguvu ya Mungu Mtulizaji: ndiye anayerudisha na kuimarisha katika imani taifa lake akilifanya mwenye nguvu na imara (1Pt 5,10-11).

Maneno ya kitulizo, wakati Mtaguso Vatikano 2 ulipokaribia kuisha, ni alama za matumaini katika Eklezya ya dunia nzima. Padri Giovanni alitambua mahitaji ya "kuamini na kutumaini pamoja", ya kuishi imani katika matumishi mbalimbali ya Eklezya.

Utumishi wa kituliza, ginsi alionjwa na Padri huyo, watusukuma kwa fazila ya upokelevu wa taifa tunaloalika lipokee Enjili; watusukuma pia kuelewa maisha na 'luga' zake (hata zile zisizo wa maneno); tena watusukuma kuhatarisha uzima, bora tuishi, kwa usikivu-moyoni, huzuni, misongano ya roho, maulizo makuu ya mwanadamu katika hali yake na ya jumla ya watu, na nyakati za sasa.

# Siku ya kenda (17.08.'24)

*Kusali sikuzote*

## Somo fupi

Eb 13,7-9a

Wakumbukeni waongozi wenu waliowaletea nyinyi Neno la Mungu. Fikirini kwa uangalifu mwisho wa namna yao ya kuishi, fuateni imani yao. Yesu Kristu ni yuleyule jana na leo na hata milele ! Msivutwe na mafundisho ya namna mbalimbali na ya kigeni.

## Somo la kixaveriano

"Barua kwa wazazi" ya Vittorio Faccin, mtawa na shaidi

(*Epistolario*, Roma 2024, 189; Baraka, 22.11.1964)

*Mashahidi wapya: waombezi wetu*

Siku sita kabla ya kuuawa, frera Vittorio Faccin aliandika:

"Natumaini kama barua hii iwafikie. Afya ni njema japo magumu machache, ambayo yameisha-pita. Kwetu sasa hakuna ginsi ya kupashana habari: tunaona kiu ya uhuru, lakini uhuru huo utafika wakati gani? Kila siku ni siku ya kungoja. Kuelezea yale tuliyoyaona wakati huu haiwezekani na yatabakia moyoni mwetu sikuzote.

Mama wa Mbinguni aliyetukinga mpaka sasa kwa mwujiza, ataendelea kutukinga. Naona hakika kwamba tutatokamo salama. Sala zenu zapokelewa mbinguni. Muzidi kusali kwa ajili ya watu hawa wanyonge. Mutoe machozi miguuni mwa Mama wa mbinguni, Mama wa Mitume. Musali. Nawakumbatia wote".

## Mafikiri

Ya akina bwana Fransisko Beschi, askofu wa Bergamo

Kifo kimetia muhuri juu ya maisha mafupi na yenye maana kuu ya Mashahidi. Twaweza kusema kuhusu Vittorio, Luigi, Giovanni na Albert maandiko yaandikayo kuhusu Mashahidi wengineo: *Hawakumwibia maisha, mwenyewe aliyatolea tangu mbele*.

Luigi Carrara na wenzaka mashahidi wanatukumbusha pia wamissiomari wengi waliopandika maisha yao ya imani katika udongo wa Kongo, wakiungana na watu, karibu na wamaskini zaidi. Walikumbuka kwamba tunaitwa kushuhudia enjili na mapendo ya Mungu pale Mwenyezi alimotupandika, sivyo penginepo. Na pale tulimopandikiwa ndipo tutasema pamoja na Padri Luigi: *Tuko katima mikono ya Mungu*.

Wakati huu, kwa namna ya pekee, Eklezya inaitwa kuwa misionarya, kwa mapendo hodari yasiyotafuta sifa ya watu, bali mema tu ya wanadamu. Eklezya inapashwa kujua kuishi katika historya kwa unyenyekevu ikitumika na juhudi, ikijua kusema maneno ya ukweli hata bila kuyanena, nayo kwa wale wasiosadiki bado.

Mashahidi wapya wanaotangazwa Wenyi-Heri, ambao waliamini sala daima, sasa karibu na Mungu, watuombee sisi na Eklezya yetu nzima.

# Oroza

**Mpango wa sala** ..... 3

**Siku ya kwanza (09.08.'24)** ..... 4

*Kujitolea* ..... 4

**Siku ya pili (10.08.'24)** ..... 6

*Kufaidia Kristu* ..... 6

**Siku ya tatu (11.08.'24)** ..... 8

*Utiifu na mapendevu* ..... 8

**Siku ya nne (12.08.'24)** ..... 10

*Kupenda kwa moyo wote* ..... 10

**Siku ya tano (13.08.'24)** ..... 12

*Kudumu* ..... 12

**Siku ya sita (14.08.'24)** ..... 14

*Kindugu* ..... 14

**Siku ya saba (15.08.'24)** ..... 16

*Kujitolea kwa Maria* ..... 16

**Siku ya nane (16.08.'24)** ..... 18

*Kushurulikia* ..... 18

**Siku ya kenda (17.08.'24)** ..... 20

*Kusali sikuzote* ..... 20

Wamissionaryo Waxaveriani
Wapostulanti